TANGAZO LA SERIKALI NA. 908 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO NA MAGULIO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"dalali" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa za sokoni kwa njia ya mnada kwa niaba ya mwenye bidhaa kwa mujibu wa sheria na taratibu za soko;

"gulio" maana yake ni soko la wazi linalofanyika kwa wakati maalumu kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba;

"kamati ya wadau wa soko" maana yake ni Kamati ya wafanyabiashara iliyoundwa kutokana na Wenyeviti na Makatibu wa vikundi vidogo vidogo vya

wafanyabiashara ndani ya soko;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu Sheria Ndogo hii;

"kodi ya pango" maana yake ni kodi inayolipwa na mpangaji kwa Halmashauri kila mwezi au kila siku kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"kodi ya pango" maana yake ni kodi inayolipwa na mpangaji kwa Halmashauri kila mwezi au kila siku kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"makasha" maana yake ni vifaa maalum vya kubebea, kufungashia au kuhifadhia bidhaa au mazao na yatahusisha matenga, viroba, magunia, karatasi ngumu, masanduku ya mbao na mengine yenye asili hiyo;

"meza au kizimba" maana yake ni kitu au kifaa kinachotumika kuweka bidhaa kwa ajili ya kuuza sokoni au gulioni;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa sokoni au gulioni kwa jumla au rejareja;

"mkuu wa soko" maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa au aliyeajiriwa na Halmashauri kusimamia shughuli zote katika soko;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"soko" maana yake ni eneo maalumu la biashara lililotengwa na Halmashauri kwa matumizi ya kuuzia au kununulia bidhaa pamoja na gulio;

"ushuru" maana yake ni tozo inayolipwa baada au kabla ya kupata huduma katika soko au gulio;

"vikundi" maana yake ni vikundi vya ushirika vya wafanyabiashara au umoja wa vikundi vya wafanyabiashara vilivyosajiliwa au kuandikishwa na

kuwasilishwa katika kamati ya soko au gulio na kwa mkuu wa soko na kutambuliwa na Halmashauri;

"wadau wa soko" maana yake ni mfanyabiashara binafsi, vikundi vilivyoandikishwa katika kamati ya wadau wa soko au gulio na kuwasilishwa kwa mkuu wa soko, au vyama vya ushirika vinavyofanya shughuli za biashara katika soko;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, shirika, taasisi au kampuni ambayo imeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri; na

"mazao" maana yake ni mavuno ya shambani au maliasili yanayoingizwa kwenye soko au ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri

4. Pamoja na wajibu mwingine, Halmashauri itakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kukusanya ushuru au ada mbalimbali kutoka kwa wafanyabiashara wa masoko, minada na magulio;
(b) kuanzisha, kusimamia na kuendesha masoko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(c) kuendeleza masoko;
(d) kusimamia usafi na usalama wa masoko;
(e) kusimamia ufikishaji wa huduma za kijamii katika soko;
(f) kugawa na kupangisha soko kwa vyumba, meza au vizimba;
(g) kutenga maeneo kwa ajili ya magulio; na
(h) kusajili wafanyabiashara wote katika masoko yote ya Halmashauri.

Mkuu wa Soko

5.-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Soko atakayeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kusimamia shughuli za uendeshaji wa soko.

(2) Mkuu wa soko atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia ukusanyaji wa ushuru au ada

mbalimbali;
- (b) kusimamia usajili wa wadau wa soko kwa kushirikiana na kamati ya wadau wa soko;
- (c) kuimarisha huduma za ulinzi, maji na umeme katika masoko;
- (d) kusimamia usafi na uondoshaji wa taka katika soko;
- (e) kuhakikisha kuwa bidhaa haziuzwi kwenye eneo ambalo haliruhusiwi kwa shughuli hiyo;
- (f) kuzuia ujenzi holela katika soko; na
- (g) kutekeleza majukumu mengine yoyote yatakayoagizwa na Halmashauri.

(3) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kuajiri wakala ambaye atawajibika kusimamia uendeshaji wa soko kwa niaba yake.

(4) Wakala atakayeajiriwa chini ya aya ndogo ya (3) atasimamia shughuli za uendeshaji wa soko kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ndogo ya (1) na masharti ya mkataba wa uwakala kati yake na Halmashauri.

Kamati ya Soko

6.-(1) Kutakuwa na kamati ya wadau wa soko ambayo itaundwa na wadau wa soko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Kila kikundi cha ushirika katika soko kitakuwa na mwakilishi mmoja katika kamati ya wadau wa soko.

(3) Kamati ya wadau wa soko itatakiwa kuweka utaratibu maalum wa kuwapata viongozi wake, kuwaondoa madarakani na uendeshaji wa shughuli zake na kuuwasilisha kwa Halmashauri.

(4) Vikao vya Kamati ya wadau wa soko vitafanyika mara moja kila mwezi.

(5) Mkuu wa Soko atakuwa Katibu katika vikao vyote vya Kamati ya wadau wa soko.

(6) Muda wa wajumbe wa kamati ya wadau wa soko kuwa madarakani ni miaka mitatu.

Majukumu

7. Kamati ya wadau wa soko itakuwa na majukumu

ya Kamati

yafuatayo:

(a) kuhakiki biashara zinazoendeshwa katika soko;
(b) kuboresha ustawi wa wadau wa soko;
(c) kuhakikisha uwepo wa nidhamu katika shughuli za soko;
(d) kuhakikisha wadau wote wa soko na gulio wanalipa ushuru au ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(e) kukuza na kuendeleza mfumo wa biashara;
(f) kuhakikisha kila eneo la mdau na soko kwa ujumla linakuwa safi muda wote;
(g) kutekeleza kazi nyingine watakazoelekezwa na mkuu wa masoko kulingana na Sheria ndogo hii; na
(h) kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo masokoni.

Kamati ndogo

8.-(1) Kamati ya wadau wa soko itaunda kamati ndogo zenye wajumbe wanne kutoka miongoni mwa wajumbe wa kamati ya wadau wa soko ambazo ni:

(a) Kamati Ndogo ya Miundombinu na Usafi;
(b) Kamati Ndogo ya Utawala na Biashara; na
(c) Kamati Ndogo ya Ulinzi na Usalama.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), kamati ya wadau wa soko inaweza kuunda kamati ndogo yoyote kwa kadri itakavyoona inafaa.

Vikao vya Kamati ya wadau wa soko

9.-(1) Kutakuwa na kikao cha kamati ya wadau wa soko kitakachofanyika mara moja kila mwezi ambapo Mwenyekiti atachaguliwa miongoni mwa wajumbe wa kamati hiyo.

(2) Kamati ya wadau inaweza kukutana kwa jinsi itakavyoona inafaa nje ya kikao cha kisheria kwa ajili ya kutekeleza maazimio yaliyoainishwa katika kikao cha kamati ya wadau wa soko.

Ushuru wa kupakua na

10. Kutakuwa na ushuru utakaotozwa kwa kila

kupakia mizigo

chombo cha usafiri kitakachoingia ndani ya eneo la soko au barabara za soko kwa ajili ya kupakua au kupakia bidhaa kwa kuzingatia viwango viilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Usajili wa wadau

11. Mtu yeyote anayekusudia kufanya biashara katika eneo la soko atatakiwa kusajiliwa na Mkuu wa Soko akishirikiana na kamati ya wadau wa soko kwa lengo la kumtambua na kumworodhesha katika rejesta ya wadau wa soko.

Utolewaji wa kibali kwa biashara ambazo hazikuwepo

12. Mtu au mfanyabiashara yeyote ambaye anakusudia kufanya biashara ambayo awali haikuwepo au haikuwa na eneo ndani ya soko ataomba kibali kwa Halmashauri na atapaswa kuzingatia masharti ya aya ya 11.

Uteuzi wa wakala

13.-(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote au kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kuwa wakala ambaye atawajibika kukusanye ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Kufuta kibali

14.-(1) Mkuu wa soko anaweza kufuta kibali kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hii, baada ya kutoa notisi ya siku thelathini, endapo mwenye kibali hicho-

(a) atakuwa na malimbikizo ya ushuru;

(b) atakuwa amesimamisha shughuli zake kwa miezi

mitatu bila taarifa;

(c) atakuwa na mwenendo unaokiuka masharti ya Sheria Ndogo hii;

(d) atawashawishi wafanyabiashara wengine kutofuata Sheria Ndogo hii au kusababisha uvunjaji wa amani; au

(e) atatumia chumba, kibanda, meza au kizimba alichopanga kinyume na madhumuni ya kufanyia biashara kama yalivyoainishwa kwenye mkataba wa upangishaji au maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri.

(2) Mfanyabiashara ambaye hataridhika na uamuzi wa kufutiwa kibali anaweza kuwasilisha pingamizi lake kwa Mkurugenzi katika kipindi cha siku kumi na nne tangu tarehe ya kufutiwa kibali.

(3) Baada ya kupokea pingamizi, Mkurugenzi atatakiwa kutoa uamuzi wa pingamizi ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea pingamizi husika.

Wajibu wa mfanyabiashara

15. Kila mfanyabiashara katika eneo la soko atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kusajiliwa na Mkuu wa soko katika rejesta ya wadau wa soko;

(b) kulinda na kuhifadhi miundombinu ya soko;

(c) kufanya biashara katika maeneo yanayoruhusiwa;

(d) kufanya usafi katika eneo lake la biashara;

(e) kulipa ushuru kwa wakati;

(f) kutobandika au kutobandua tangazo bila idhini ya Mkuu wa soko;

(g) kutotumia lugha ya matusi, kuudhi au kashfa katika eneo la soko;

(h) kushiriki usafi wa jumla wa soko;

(i) kutoweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya eneo la soko;

(j) kutofanya shughuli za kisiasa katika eneo la soko;

(k) kutotupa taka ovyo au kutiririsha maji machafu;
(l) kutowasha moto maeneo yasiyohusika ndani ya soko; na
(m) kuheshimu masharti ya upangaji aliyopewa na Halmashauri na maelekezo atakayopewa na Halmashauri, Mkuu wa soko na kamati ya wadau wa soko.

Ujenzi na ukarabati

16. Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya ujenzi, ukarabati au marekebisho ya chumba, kibanda, meza au kizimba pasipo idhini ya maandishi ya Halmashauri.

Muda wa biashara

17.-(1) Soko litakuwa wazi siku zote kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Mkuu wa Soko, kwa kushauriana na Mkurugenzi, anaweza kufunga soko kwa ajili ya matengenezo au sababu nyingine yoyote ya dharura pale itakapoonekana inafaa.

(3) Isipokuwa kwa sababu nyingine za dharura, Mkuu wa soko hatakuwa na mamlaka ya kufunga soko kwa sababu za matengenezo isipokuwa tu baada ya kutoa notisi ya siku saba kwa wadau wa soko kuhusu kusudio la kufunga soko kwa ajili ya matengenezo.

Kodi ya upangishwaji

18.-(1) Kila mfanyabishara katika soko atalipa kodi ya upangishwaji kizimba au kibanda kwa mujibu wa mkataba wa upangishwaji.

(2) Kodi ya upangishwaji italipwa kwa Halmashauri au wakala kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Halmashauri inaweza, kwa makubaliano maalum, kumruhusu mtu yeyote kujenga banda la biashara katika eneo la soko.

Usimamizi wa magari

19.-(1) Magari yote yanayotumika kusafirisha mazao au bidhaa kwa ajili ya soko yatashusha bidhaa katika maeneo yaliyoainishwa kwa shughuli hiyo.

(2) Mkuu wa soko atakuwa na mamlaka ya kupanga na kusimamia idadi ya magari yatakayoruhusiwa kushusha bidhaa au mazao sokoni.

(3) Gari lolote litaondolewa kutoka sehemu iliyotengwa endapo itabidi kufanya hivyo na Mkuu wa soko.

Kibali cha minada na magulio

20.-(1) Minada ya mazao, nguo na bidhaa nyingine itaruhusiwa kufanyika kwenye masoko kwa kibali maalum cha Halmashauri.

(2) Halmashauri inaweza kutoa kibali maalum cha kufanyika kwa magulio katika maeneo yatakayotengwa na Halmashauri na kitakuwa kama kinavyoonekana kwenye Jedwali la Tatu.

Usafi wa soko

21.-(1) Kila mfanyabiashara anayefanya biashara katika eneo la soko atawajibika kuweka eneo lake katika hali ya usafi wakati wote.

(2) Mkuu wa soko kwa kushirikiana na kamati ya wadau wa soko atasimamia usafi wa jumla wa soko siku ya jumamosi ya mwisho wa mwezi.

(3) Kila mfanyabiashara atatakiwa kuzingatia kanuni za afya.

Uingizaji wa bidhaa sokoni au gulioni

22.-(1) Bidhaa zote zitakazoingizwa katika soko au gulio zitatakiwa kuhifadhiwa kwenye makasha maalumu ya kusafirishia bidhaa.

(2) Ni marufuku kwa mkulima, mfanyabiashara, dalali au mtu mwingine yeyote kuingiza sokoni au gulioni bidhaa zilizoharibika.

(3) Mtu yeyote atakayeingiza sokoni bidhaa zilizofungwa kwa majani atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Mifugo kutoingizwa sokoni

23. Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza mifugo sehemu yoyote ndani ya soko, magulio au minada isipokuwa sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri

kwa ajili ya biashara ya mifugo.

Minada

24.-(1) Mazao yatakayoletwa sokoni kwa ajili ya kuuzwa kwa mnada yatapokelewa na dalali atakayeteuliwa na wafanyabiashara na kukubaliana na kamati ya soko.

(2) Dalali aliyeteuliwa atauza mazao hayo kwa mnada katika eneo lililotengwa na Halmashauri kwa shughuli hiyo.

Biashara ya kutembeza

25. Mtu yeyote hataruhusiwa kutembeza bidhaa ndani ya soko bila kibali cha Halmashauri.

Tahadhari ya moto

26. Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya shughuli yoyote inayohusisha matumizi ya moto isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Halmashauri.

Uuzaji wa pombe

27. Mfanyabiashara yeyote hataruhusiwa kuuza pombe ndani ya soko, gulio, mnada bila kibali na leseni ya vileo iliyotolewa na Halmashauri.

Marufuku

28. Ni marufuku kwa mtu yeyote:

(a) kubandika au kubandua tangazo lolote bila ya idhini ya Mkuu wa Soko;
(b) kuweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya eneo la soko;
(c) kufanya shughuli za siasa ndani ya soko;
(d) kuharibu miundombinu ya soko;
(e) kutumia lugha ya matusi ndani ya soko;
(f) kufanya shughuli yeyote kwenye eneo ambalo haliruhusiwi au halijatengwa kwa shughuli hiyo;
(g) kutupa taka ovyo au kutiririsha maji machafu;
(h) kuwasha moto maeneo yasiyohusika ndani ya soko; na
(i) kufunga chumba cha biashara kwa madai ya kukitumia kama stoo au matumizi mengine yasiyoainishwa katika mkataba au leseni;

Makosa na adhabu

29. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na

kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha Kosa

30. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 10)*

A: USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA MIZIGO SOKONI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Ada kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba kilogram 500 | - |
| 2 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 1 | - |
| 3 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 1.5 | 5000 |
| 4 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 2 | 10,000 |
| 5 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 3 | 12,000 |
| 6 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 4 | 15,000 |
| 7 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 5 | 16,000 |
| 8 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 7 | 18,000 |
| 9 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Tani 8 hadi 10 | 20,000 |
| 10 | Chombo cha usafiri chenye uwezo wa kubeba Zaidi ya tani 10 | 25,000 |

*Tangazo La Serikali Na. 908 (Linaendelea)*

B: USHURU WA MAEGESHO SOKONI

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru kwa siku (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Lori kubwa lenye uwezo wa kubeba tani 5 na kuendelea | 1,000/= |
| 2. | Lori la kati lenye uwezo wa kubeba tani 5 | 600/= |
| 3. | Gari dogo | 500/= |
| 4. | Pikipiki | 500/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 18(2))*

ADA YA KUPANGISHA ENEO

| Namba | Aina ya eneo au chanzo | Ada kwa mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kizimba | 10,000 |
| 2 | Banda vya kuku | 10,000 |
| 3 | Mama au Baba lishe | 10,000 |
| 4 | Vioski au mabanda ya Mitumba na Bucha | 30,000 |
| 5 | Duka | 50,000 |
| 6 | Stoo | 150,000 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 20(1))*

KIBALI CHA KUTUMIA SOKO

1. Jina la Mwombaji …………………………………………………………
2. Anuani ya mwombaji ………………………………………………………
3. Kibali cha …………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
4. Eneo ambalo kibali hicho kitatumika ……………………………………..
   ………………………………………………………………………………
5. Muda wa Kibali ni kuanzia tarehe……………………hadi tarehe…………
6. Masharti ya kutumia kibali hicho……………………………………………..
   a) ………………………………………………
   b) ………………………………………………

*Tangazo La Serikali Na. 908 (Linaendelea)*

c) ………………………………………………
d) ………………………………………………
e) ………………………………………………

7. Tarehe ya kikao iliyoidhinisha kibali………………………………………… Muhtasari Na.……………

8. Imesajiliwa na:
Jina ………………………………………
Saini…………………………………….. ………………………………
Mkuu wa Soko Saini ya Mwombaji
Tarehe …………………………………. Tarehe ……………………
Mhuri……………………………………

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 30)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi……………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya……………………………………..……. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, kwamba mnamo tarehe: …… ya Mwezi:….…. Mwaka: ……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya ….. ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlim ba ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe:…...... ya Mwezi:………… Mwaka:…………..
Jina:………………………………..…………………….
Saini:…………………………..……………………………

MBELE YANGU :
Jina: ……………………………………..……………………
Cheo: ……………………………………………………..…….
Saini: …………………………………………………………
Tarehe: ……………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Mlimba imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba uliofanyika Tarehe 27 Mwezi Oktoba Mwaka 2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

ENG. STEPHANO B. KALIWA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

INNOCENT SIMON MWANGASA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*